TANGAZO LA SERIKALI Na. 1056 la tarehe 20/12/2024

SHERIA YA MISITU,

(SURA YA 323)

# NOTISI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 23(1))*

NOTISI YA KUSUDIO LA KUTANGAZA ENEO LA MSITU WA IYUMBA KUWA MSITU WA HIFADHI WA TAIFA IYUMBA YA MWAKA 2024

Jina

**1**. Notisi hii itajulikana kama Notisi ya Kusudio la Kutangaza Eneo la Msitu wa Iyumba kuwa Msitu wa Hifadhi wa Taifa Iyumba ya Mwaka 2024.

Eneo linalopendekezwa kutangazwa

**2**. Eneo la msitu lililo ndani ya mipaka iliyoainishwa katika Jedwali linapendekezwa kutangazwa kuwa Msitu wa Hifadhi wa Taifa Iyumba.

Madhumuni ya tangazo

**3**. Madhumuni ya kupendekezwa kutangaza Msituwa Hifadhi wa Taifa Iyumba ni-

(a) kulinda eneo lililo hatarini la misitu ya uwanda wa juu wa miombo na ardhi oevu ambalo linatambulika kwa thamani yake ya juu ya baioanuwai, lenye upekee wa mimea na wanyama, ikijumuisha aina za mimea na wanyama walio hatarini kutoweka; na

(b) kulinda eneo la msitu na matumizi endelevu ya rasilimali za misitu katika eneo la msitu huo.

Uhalali wa Notisi

**4**.-(1) Notisi hii itakuwa halali kwa muda wa siku tisini kuanzia tarehe ya kuchapishwa katika Gazeti la Serikali.

(2) ) Ndani ya kipindi hicho cha siku tisini, mtu au kundi la watu au mwakilishi wao anaweza, kwa maandishi kuwasilisha pingamizi, maoni au madai ya

haki yoyote inayotokana na sheria za kimila kuhusiana na ardhi au mazao ya msitu au haki yoyote iliyoainishwa kwenye sheria nyingine katika eneo ambalo linapendekezwa kutangazwa kuwa Msitu wa Hifadhi wa Taifa Iyumba.

Uwasilishaji wa pingamizi

**5**. Pingamizi, maoni au madai yoyote dhidi ya kusudio la kutangaza eneo la Msitu wa Iyumba kuwa Msitu wa Hifadhi wa Taifa Iyumba, yawasilishwe ndani ya siku tisini kuanzia tarehe ya kuchapishwa kwa Notisi hii kwa anuani ifuatayo:

Katibu Mkuu,
Wizara ya Maliasili na Utalii,
S.L.P 1351,
DODOMA.

*Tangazo la Serikali Na.1056 (Linaendelea.)*

JEDWALI


*(Limetengenezwa chini ya aya 2)*

WILAYA YA ILEJE

MSITU WA HIFADHI WA TAIFA IYUMBA

Makadirio ya eneo: Hekta 109 au Kilometa za Mraba 1.10 Unakopatikana na Mipaka

Eneo lote la hifadhi awali chini ya Eneo la Msitu wa Iyumba unaopatikana Wilaya ya Ileje katika Mkoa wa Mbeya kama lilivyochorwa katika Ramani Na. Jb 2304 (Skeli 1:5000) iliyohifadhiwa na Mkurugenzi wa Upimaji na Ramani na lenye mipaka ifuatayo:




Dodoma
11th November, 2024

PINDI HAZARA CHANA,
*Waziri wa Maliasili na Utalii*